# SURA YA TISA

KUKUZA UTARATIBU WA MUNGU KWA MAISHA YA KIFAMILIA

Ni njia gani bora kabisa ya kuonyesha upendo wa Yesu Kristo katika maisha yako? Mungu amekupatia njia maalum ya kuonyesha upendo huo. Nyumbani ndipo pahali pa kwanza pa kudhihirisha upendo wa Kristo kwa kuwa ndoa inalinganishwa na uhusiano wake kwa kanisa lake. Neno la Mungu lasema kuwa tunaweza kuhudumu kote nchini, lakini tukikosa kuhudumia familia zetu, itakuwa vigumu kutenda huko nje. Ushahidi wetu utaongezeka pindi tu mahusiano yetu nyumbani yataongezeka katika upendo (1 Timotheo 3:4-5).

<u>Uchangukaji wa Mamlaka</u>

Tunapolifahamu jambo hili, tunaweza kuona ni wapi adui anataka kushambulia zaidi – familia. Akiweza kuvunja familia pahali ambapo upendo wa Kristo unatakiwa kudhihirishwa, basi atakuwa ameharibu ushuhuda wa Bwana Yesu Kristo kote ulimwenguni. Ni katika familia watoto wanapaswa kufundishwa nidhamu katika Bwana Yesu. Pahali ambapo wanaume na wake zao wanatakiwa kufanya kazi pamoja katika upatanifu wa Bwana. Katika nchi hii leo uchangukaji wa mamlaka umekuwa ukifanyika. Watoto hawafundishwi kuenzi na kuheshimu. Wake wengine hawawaenzi na kuwaheshimu waume zao nao wanaume hawamuenzi Mungu.

Kuna maeneo matano makuu ambapo mamlaka hutumika: nyumbani, kanisani, serikalini, katika mahusiano ya mwajiri na mwajiriwa na Mungu. Shetani anataka kuchangua mfumo wa mamlaka uliojengwa kwenye kanuni za Mungu na kuuzatiti ulio wake. Mfumo wa Shetani wa mamlaka hufanya kazi kwa kuiinua nafsi yako dhidi ya kanuni za Mungu, unajiteuwa wewe mwenyewe kuwa mamalaka.

2 Timotheo 3:1-7  yaelezea kinachofanyika katika ulimwengu leo.
"*Lakini ufahamu neno hili, ya kuwa siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari" (*Tuko katika nyakati za mwisho*) "Maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiotii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio safi, wasiowapenda wa kwao, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wsiojizuia, wakali, wasiopenda mema, wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake, hao nao ujiepushe nao. Kwa maana katika hao wamo wajiingizao katika nyumba za watu na kuchukua mateka wanawake wajinga wenye mizigo ya dhambi, waliochukuliwa na tamaa za namna nyingi, wakijifunza siku zote, ila wasiweze kabisa kuufikia ujuzi wa kweli*."

Tunapoangalia mazingira yetu tunaziona sifa hii zote zikijitokeza katika jamii yetu ya sasa. Zimo nyumbani mwetu, shuleni na makanisani. "*wenye mfano wa utuwa, lakini wakikana nguvu zake.*" Kuna watu wajiitao wakristo lakini hawalishughulikii alisemalo Mungu katika neno lake. (Hawataki kulipokea au kulifanya, yawezekana wanalitaka lakini hawataki kulitenda. Jambo hili huzikana nguvu za Mungu. Nguvu za Mungu hutembea tunapokubali kwa imani.

Imani hufanya kazi vipi? Imani hutenda kwa kusikia na kusikia neno la Mungu. Hufanya kazi tunapokubali kanuni za Mungu na kuzitenda. Tusiwe wasikizaji wa neno pekee bali watendaji

pia. Nguvu za Mungu huanza kutembea wakati watu wa Mungu, kwa imani na kwa kulikubali neno lake kuamini Mungu kuwa atafanya alisemalo.
Yuda ni kitabu chenye nguvu kinachotaja siku za mwisho. "*Kadhalika na hawa, katika kuota kwao huutia mwili uchafu,hukataa kutawaliwa, na kuyatukana matukufu* (mamlaka ya Mungu) Mamlaka ya Mungu yawe ni ya kikristo au la hubaki mamlaka yake kulingana na neno lake. Mungu hufanya kazi kuyapitia, lakini yanakataliwa. Hayaheshimiwi na kuenziwa hata na wakristo. Hata ikiwa jambo hili linadhalalisha kanuni za Mungu. Mungu alisema lingetokea katika nyakati za mwisho. Tunatakiwa kujihadhari na kutambua kuwa mamlaka yote yawe ya kikristo au la yanatokana na Mungu. Tunatakiwa kuyaheshimu na kuyaenzi.

2 Petro 2:9 kuendelea pia na Warumi 13:1-2 hudhihirisha na kushughulikia kanuni hizi. Ni vyema kujisomea.

Yesu Kristo pekee ndiye atakayeifanya ndoa ishikamane. Ni muhimu abaki kuwa nguzo kwa mshiriki ndoa mmoja hata ikiwa anatakiwa kuwa nguzo kwa washiriki wote wawili. Jambo hili litafanyika kulingana na neno la Mungu pale ambapo mshiriki mmoja anamtafuta Mungu.

Nguvu ziendeshayo Familia.

Hizi ni baadhi ya nguvu zinazofanya kazi katika familia: watu wawili katika ndoa hujumuisha mahusiano matatu, kwa maana mtu aingiapo katika ndoa hajitoi tena kwake peke yake kwa kuwa ana mwenzi wa ndoa na ndoa anayoifikiria. Kwa hivyo mahusiano matatu hupatikana.

Kifungua mimba azaliwapo, mahusiano saba hutokea

1) Mke na mume
2) Mume na mke
3) Mume na mtoto
4) Mke na mtoto
5) Mtoto na baba
6) Mtoto na mama
7) Mtoto na ndoa

Kuna mahusiano saba yanayojitokeza wakati kifungua mimba huzaliwa. Mtoto mwingine anapozaliwa kuna kuwa na mahusiano kumi na matano.Mtoto watatu anapozaliwa, husababisha familia kuwa na mahusiano thelathini na mawili. Kuna kuongezeka.

Watu hushindwa sababu za ndoa kusambaratika. Ukikosa kumpa Yesu Kristo nafasi ya kustawisha ndoa pamoja na yale mahusiano thelathini na mawili basi utayapata magumu. Fikiria juu ya watu watano wanaojitafutia njia,vijigurudumu vyao vikizunguka na kuridhisha tamaa zao. Hivyo, ni vizuri kuweka kanuni nyumbani ambazo zinatambuliwa na kutekelezwa.
Hatuwezi kuyaachilia mahusiano haya yachukuwe njia zao peke yao. Hatuna budi kuchagua mwongozo utokanao na Mungu. Unaweza kuichagua njia ya mwanadamu ya kuyafanya mambo lakini uishie kuwa na njia 32 tofauti.

Ulipokuwa peke yako ulifanya lolote ulilolitaka. Ulikuwa wakati mzuri kwa kuwa hakukuwa na yeyote mwingine aliyehusika. Kama tulivyotaja awali pindi tu mtoto wa kwanza anapozaliwa marekebisho mengi hayana budi kufanyika katika familia. Mama akimshughulikia zaidi mtoto

wake wakati mwingine mumewe huhisi kuwa hapendwi tena. Wakati mwingine baba na kitoto chake cha kike wakiwa na uhusiano  na uhusiano huu wa karibu sana, mke huanza kuhisi hatakiwi tena.

**Kanuni za mamlaka kutoka kwa Mungu**

Tukiyafahamu yale yaliyodhihirishwa awali tutaziweka kanuni fulani chini. Huu ndio mpangilio wa kanuni za mamlaka ya  Mungu nyumbani.

"*Mnifuate mimi kama mimi ninavyomfuata Kristo. Basi nawasifu, kwa sababu mmenikumbuka katika mambo yote, nanyi mmeyashika yale mapokeo vile vile kama niliyowatolea. Lakini nataka mjue ya kuwa kichwa cha kila mwanamume ni Kristo, na kichwa cha kila mwanamke ni mwanamume, na kichwa cha Kristo ni Mungu* (1 Wakorintho 11:1-3) Haya ndiyo mamlaka ya Mungu na mpangilio wa nyumba (familia)"

"*Ninyi watoto watiini wazazi wenu, maana jambo hili lapendeza katika Bwana*." (Wakolosai 3:20) Huu ndio mfumo wa mamlaka. Kichwa cha watoto ni wazazi.

Yesu Kristo alikuwa chini ya mamlaka ya Mungu Baba wakati wa maisha yake yote hapa duniani. Hakulifanya wala kulisema lolote ambalo hakuelezwa na Babake. Hakuja kuyatenda mapenzi yake mwenyewe ila mapenzi ya Babake. Yesu ni mfano mzuri wa kuigwa katika maisha yetu wa namna tunavyopaswa kuyatii mamlaka yaliyo juu yetu.

Jambo hili hufanyikaje? Kristo ndiye kichwa cha mwanamume. Ndiye Bwana wa familia. Mambo yote hayana budi kufuata majira yake katika familia.

Mwanamume ana wajibu gani? Ndiye kichwa cha mwanamke. (1 Wakorintho 11:3) ndiye mwenye cheo cha juu kabisa cha mamlaka kwa watoto wake.

Mwanamke ana wajibu gani? Mwanzo 2:1 yasema, "*Bwana Mungu akasema, si vyema huyu mtu awe peke yake, nitamfanyia  msaidizi kwa kufanana naye*." Anatakiwa kuwa msaidizi wa mumewe. Mamlaka ya pili ni juu ya watoto na anayetawaliwa na mwanamume. Inamaanisha nini kutawaliwa na mwanamume? Inamaanisha kunyenyekea, kumheshimu, kumuenzi, kumsifu, kumpenda na kumtukuza. Hii ni kanuni muhimu ambayo haizingatiwi siku hizi. Miondoko mingi inayoasi imetupilia mbali utaratibu wa mamlaka uliowekwa na Mungu.

Katika mwanzo 3:16 Bwana Mungu alikuwa akiongea na Hawa baada ya kuanguka kwao. Utaratibu wazi ulibuniwa kama matokeo ya kutotii kwake. Atakuwa chini ya mamlaka ya mumewe naye atatawala juu yake. "*Akamwambia mwanamke, hakika nitakuzidishia uchungu wako, na kuzaa kwako; kwa utungu utazaa watoto; na tamaa yako itakuwa kwa mumeo, naye atakutawala!*" (Mwanzo 3:16)

Wanawake wanaposikia kuwa kuna mmoja anayetawala juu yao, kila  aina ya bendera nyekundu hupepea. Vile vile kwa wanaume. Si desturi ya mwanamume kuwa chini ya mamlaka.Dhambi gani ilitendeka`katika bustani ya Edeni. Hawa alikuwa na tamaa gani? Alitaka kuwa kama

Mungu. Shetani alifanya dhambi gani? Alitaka kuwa kama Mungu. Tunauona kutoka mwanzo uasi dhidi ya Mungu na mamlaka yake.

Mwanzo 3:12 yaelezea sehemu ya laana hata ikiwa tunajua tumekombolewa kutokana na laana ya sheria kupitia Yesu Kristo na kufanyika warithi wa ahadi zote za Ibrahimu. Hizi ni ahadi za utele kwa kila njia na katika mahusiano yetu. Lakini haiondoi kanuni za Mungu kuhusu mamlaka. Kukombolewa kutokana na laana hakutuweki huru kulifanya lolote tulitakalo. Tunaenda sasa kulingana na kanuni zilizowekwa na Mungu.

Mungu ametuwekea kanuni kama baraka kwetu. Hii ndio sababu ametupa mwelekeo huu na hili ndilo kusudi la sheria. Tulipowekwa sawa kupitia Yesu Kristo na kumpokea kama Bwana na mwokozi, sheria sasa inakuwa mwongozo ili tuweze kupata baraka zote zilizoahidiwa Ibrahimu.

**Utaratibu wa Mungu.**

Tunapotii alisemalo Mungu, maisha ya ukamilifu wake huanza kutujaa na kutuongoza. Tunapata ufanisi nyumbani mwetu, katika familia zetu, kifedha, kimwili na katika kila nyanja ya maisha yetu. Tunamwamini kufanya alilosema atalifanya.

*"Enyi wake, watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu, kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha kanisa; naye ni mwokozi wa mwili. Lakini kama vile kanisa limtiivyo Kristo vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo* (Waefeso 5:22-24) Wake, kulingana na utaratibu wa Mungu, Wanapaswa kutawaliwa na waume zao. Sio Mungu. Hatusemi kuwa mwanamke hatakiwi kuwa na uhusiano na Yesu Kristo. Hakika kitakachomshikilia katika utaratibu huu ni uhusiano wake na Yesu .Katika utaratibu huu mume wala si mke anawajibika kwa Mungu. Mke anawajibika kwa mumewe(soma1 Petro 3:1-4) Wakati mke anaanza kumwita mumewe 'Bwana na kumfanya vile, kutii kwake neno la Mungu kunamwezesha mumewe kumuenzi Mungu.

Utaratibu huu wakati mwingine hutumiwa vibaya ,wakati mwingine mwanamke ana haki ya kutaka kushughulika na jinsi jambo lilivyotendeka, lakini utaratibu hauna makosa.Ni utaratibu wa Mungu.Lililo baya ni njia wanaume wengine wanavyotumia utaratibu huu. Nimeshuhudia wanaume wakichukua utaratibu huu na kusema "Mimi ndimi mamlaka, bwana na mtawala katika familia hii" na kumdhulumu mkewe. Anasahau mamlaka halisi katika nyumba ni Mungu. Lakini bado anawajibika kwa Yesu Kristo jinsi anavyofanyiza kazi mamlaka hayo . Hapo ndipo tumaini la mwanamke hupatikana .Ifikapo hapa kulingana na utaratibu wa Mungu , mke asiasi lakini Mungu anafanya hasa analolisema.Mungu anamwadhibu mume.Wake , aminini na mtii na mtayaona matokeo .

Watoto wakati wote ambao ni watoto wako chini ya mamlaka.Mume ndiye mamlaka katika familia anapoongozwa na Kristo.Kuachilia mamlaka kumfikia mtoto kwa njia mbili au tatu hutatanisha.Mtoto hajui kiongozi wake ni nani.Hapo ndipo mwanamke anapaswa kusaidia mumewe ili afanye analopaswa kufanyia watoto wake .Anapokuwa mwaminifu na mtiifu kwa njia ya Mungu, kunyenyekea kwa mumewe katika kila jambo , basi Mungu atamficha na atakuwa chini ya ulinzi wake.Mungu alimuenzi Sara kwa njia hiyo.

Utaratibu wa mamlaka katika familia (1 Wakorintho 11:3).

1. Mungu
2. Kristo
3. Mwanaume
4. Mwanamke
5. Watoto

Bwana wa familia ni Kristo nayo familia yapaswa kuenenda kulingana na kanuni za Mungu .Mume ndiye mwavuli ama ulinzi wa familia yake .Mke na watoto wanakingwa na mwavuli huo.Kazi ya mwavuli ni gani? Ni ngao ikingayo familia yake kutokana na hila za adui.Wake wanapokaa chini ya ulinzi wa waume zao basi watalindwa.

Mambo huwa shwari ambapo mume yu chini ya mamlaka ya Kristo , mke yu chini ya mamlaka ya mumewe nao watoto wako chini ya baba yao .Mara nyingi mke atatoka chini ya mamlaka hayo.

Katika Waefeso 5:28-33 mume anaagizwa kumpenda mkewe kama mwili wake mwenyewe sababu ikiwa, wanaume ni wenye ubinafsi(hufikilia nafsi yao pekee) Jambo hili linasababisha Mungu kuwaagiza kupenda.Mke naye katika busara ya Mungu anaagizwa kuheshimu na kuenzi mumewe kama kwa Bwana.Kwa nini? Kwa sababu Bwana anajua jambo lililogumu sana kwa mke ni kuheshimu na kuenzi. Waliumbwa kuwa wasaidizi wa waume zao, lakini aghalabu hawaridhiki kuwa wasaidizi tu. Wanataka kuongoza. Mke anapoondoka kutoka kwenye mamalaka ya mumewe mume mara nyingi husema, "Sawa, endelea." Atakuwa akimpatia mkewe majukumu ikiwa mke anataka kuyachukua. Kutoka hapo mwavuli unaanza kutoboka kwa sababu mume hachukui majukumu yake na aliruhusu mkewe kuyachukua.

Mke anapotoka chini ya mamlaka, basi adui anamjia moja kwa moja. Mizigo na shinikizo ambazo hakuumbiwa zinaanza kumwaathiri. Watoto nao huasi. Watafanya vile mama anavyofanya. Mama ni muhimu sana katika utaratibu wa Mungu kwa sababu ana uwezo wa kushika mume na watoto pamoja.

Mume akiwa hajaamini basi Bwana ameishughulikia hali hiyo. Tazama 1 Wakorintho 7:14. Neno linasema kuwa watoto wanatakasika au kuwa watakatifu kwa sababu ya mwenzi anayeamini. Mungu anasema, "Naheshimu utaratibu wangu hata ikiwa mume hajaamini."

Wake, mmepewa waume zenu kama mamlaka juu yenu. Haijalishi kama mumeo anaamini au hajaamini. Yeye ni mumeo kutokana na hayo naye Mungu anasema, *"Nimemwita mumeo na nimemfanya kichwa*." Mke akiwa mwaminifu na mtiifu kwa mumewe kama kwa Bwana, Mungu naye anasema, "Nitakuenzi" Fauka ya hayo watoto wanafanyika watakatifu.

Agahalabu mke husema, "Mume wangu ana matundu mengi katika mwavuli wake. (yeye ni mwovu n.k) sioni vile ninaweza kuishi naye tena." Huu ni ucheshi ikiwa si ukweli. Kuna hatari mke akichukua mtizamo huu hasi wa kuondokea ulinzi wa mumewe. Atakuwa akifikiria kuwa mumewe hajamkimu kwa kile akitakacho kulingana na uongozi wa kikristo

lakini wakati huu wote Mungu amemtambua kama mamlaka. Mke anapolitwaa jukumu hili kutokuwa kwa mumewe, basi anajitwiza mizigo yote. Jambo hili linampelekea kuwa na mitizamo sumbufu kwa mumewe.

“Yeye hujipendekeza tu, hafanyi chochote vizuri; amenisikitisha pamoja na watoto na nimechukua majukumu yake yanayowahusu. Hapatikani.

Mke amemwangalia kwa dharau (akikusudia au bila kukusudia) au aanza kuwa msukumizi wa dini. Baada ya muda mfupi uasi ule unafanyika nguvu za kutenganisha katika ndoa. Agahalabu wanawake wanatamani sana kumfuata Bwana lakini wanahisia kuwa hawawezi himili tena. Kwa nini? Sababu wameondokea mamlaka ya waume zao kwa hivyo shinikizo zote huwapata. Wanaweza kuondoka. Neno la Mungu lasema kuwa ikiwa mwenzi asiyeamini anakubali kukaa, basi mwenzi anayeamini na akae. (1 Wakorintho 7:10-14)

Baraka zitatujia tutakavyoutii utaratibu wa Mungu. Hizi ndizo sheria zake. Katika maisha haya kuna mipango mbalimbali lakini huu ndio mpango wa Mungu. Usitamauke unapogundua kuwa umekosa kufuata baadhi ya kanuni hizi, sababu hakuna ndoa timilifu. Hata hivyo waliooana wanatakiwa kuwa pamoja huku wakitamani kutii na kufuata mpango wa Mungu katika ndoa iliyotimilifu.

**Wawili kuenziana**.

Ufunguo wa ndoa iliyo katika Bwana ni wawili kusameheana, kuenziana na kusheshimiana. Waefeso 5:21 yasema, “ *Hali mnanyenyekeana katika kicho cha Kristo.”* Kauli hii imetumiwa vibaya. Haiashirii kuwepo kwa mfumo sawa wa mamlaka. Inasema waume na wake waenende kwa kuenziana na kuheshimiana katika Bwana sababu Kristo ndiye kichwa. Utaratibu huu wa Mungu, tuliweke jambo hili wazi, si utaratibu wa uwezo. Huu ni utaratibu wa mamlaka na wajibu ambao Mungu alikusudia ndoa kufaa kama alivyotarajia.
Wakati mke anaponyenyekea kwa utaratibu wa Mungu, anaweza kujikuza na kuwa mwanamke Bwana anamtaka awe. Anaanza kuwa mbunifu wakati jambo hili linafanyika. Unafanya mahitaji ya mwanamume kukimiwa kiajabu.

Watoto wataona uhusiano mzuri baina ya wazazi wao nao watakuwa na sababu ya kumuenzi na kumheshimu Yesu Kristo. Watauona umuhimu wa Yesu wakati mama na baba wanamfuata. Familia yote inatamani kumfuata Yesu. Hii inakuwa desturi inayofurika kwa mtoto kuanza kuona upendo wa Bwana.

Enzianeni nyote wawili. Wake wastahini waume zenu kwa sababu Mungu huwaita waume. Waume wapendeni wake zenu kwa sababu Mungu huwaita wake. Mke anaweza kusema, “Sioni chochote cha kuheshimiwa na kuenziwa katika mume wangu.” Mume naye anaweza kusema, “Sioni sababu yoyote ya kumpenda mke wangu kwa sababu anafanya hili na lile.”

Tukumbuke hapa kwamba katika ndoa hakuna jambo la mtu kuwa anastahili upendo wa mwingine. Mwenzi hawezi kugeuka na kuwa vile unavyoyaka kabla ya kumheshimu na kumstahi. Kusema, “Lazima aichumie heshima na enzi” au “Lazima auchumie upendo wangu” ni makosa. Kanuni ifuatayo ya Kristo inapaswa kufanya kazi, “*Mungu aonyesha*

*pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu tulipokuwa tungali wenye dhambi*." (Warumi 5:8) Lazima tuuelewe ukweli huu. Haimchukui mume kuchumia upendo wa mkewe. Aidha haimuchukui mume kuchumia heshima na stahi kutoka kwa mkewe. Kristo, tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alitufia msalabani.

Fahamu – tulipokuwa tungali wenye dhambi. Hii inamaanisha, tulipokuwa maadui wa Mungu, wasiostahili na waliotengwa kutoka kwa Mungu kwa kila njia. Kristo alikufa ili tuwe wake. Utiifu wa Yesu kwa neno la Mungu uliwaweka huru waume kuwapenda wake zao na wake kuwaheshimu na kuwaenzi waume zao.

Ukitaka kumvuta mumeo kwa Bwana au kumvuta mkeo kwa Bwana, mpende. Mume apende naye mke aheshimu na aenzi. Hakuna anayestahili haya. Upendo wa Kristo wasema wanastahili kwa sababu Mungu anawaita wanaostahili.

Pindi tu mke anapoelewa jambo hili atatambua kuwa hakika anaweza kumheshimu na kumuenzi mumewe Mungu amemteuwa kuwa kichwa. Mara nyingi mke anasema amemchagua mume kwa hivyo anaweza kuchagua kumuacha. La! Ndoa haijajengwa juu ya upendo jinsi ulimwengu unavyoelewa. Ndoa ya kiungu inahusisha kujitolea kwa Mungu na mwenzio. Katika ulimwengu hakuna kujitolea.

**Mapenzi hayawezi kuwa msingi thabiti wa ndoa.**

Wakati wachumba wanaponijia, huwauliza sababu ya kutaka kuoana. Mara nyingi huniambia ni kwa sababu wanapendana. Hiyo ni sababu mbaya zaidi ya kuoana, Mapenzi ya ulimwengu yamejengwa juu ya ngono, kupendezwa na maumbile ya mwili, pesa, cheo, hadhi ya kijamii au kupumbazwa. Mapenzi ya ulimwengu ni haya; siku moja unapenda, siku inayofuatia unachukia. Yamejengwa kwa msingi wa mhemko, hali na mahali. Hakuna udhabiti katika mapenzi haya. Aina hii ya mapenzi haiwezi kuwa msingi thabiti wa ndoa kudumu. Lazima kuwe na kinachodhibiti ndoa.

Ndoa haijengwi katika mapenzi jinsi ulimwengu unavyofahamu. Lakini imejengwa kwenye msingi wa upendo wa Kristo na kutambua kuwa umeteuliwa (na Mungu amekupatia) mumeo au mkeo. Ulimchukua mumeo katika ndoa kama mwakilishi wa Mungu katika ndoa, kwa mazuri au mabaya. Itakuwa kwa mazuri unapotafuta kanuni za Mungu.

Sio mapenzi yanayodumisha ndoa, mbali kujitolea kwa ndoa kunadumisha mapenzi. Ni muhimu kulielewa jambo hili. Tukikosa msingi huu, basi mambo yataharibika. Jambo litakalodumisha ndoa ni watu wanaomtafuta Yesu Kristo na kufuata kanuni zake – na kutaka kufanya hivyo kwa vyovyote vile. Wanatakikwa kuifanya ndoa yao iendelee, kwa maana ndoa ya kiungu inahusisha kujitolea. Talaka si chaguo hasa kwa wakristo wawili. (1 Wakorintho 7:10-11) (Mathayo 19:1-10) (Malaki 2:11-16)

"Ikiwa hatupendani tena?" Mara nyingi nimewasikia watu wakifikia wakati wa wakusema "wanahisi" kuwa hawapatani tena. "Mwanamke niliyemwoa miaka 20 iliyopita au miaka 5 iliyopita) sio mwanamke niliyemjua. (Mwenzi mmoja amebadilika) Katika ndoa wenzi wote watabadilika kwa hivyo ndoa haiwezi kujengwa kwenye misingi ya kile ulichokiona mwanzo

kwa mwenzi wako wa ndoa. Msingi wako unapatikana uliko sasa. Msingi wa miaka iliyopita haudhibiti ndoa tena.

Unapowaza humpendi mwenzio tena, huo ndio wakati wa kuanza kujifunza jinsi ya kumpenda. Upendo wa kweli huhusisha utiifu kwa neno la Mungu. Tumeashiriwa kupendana na jambo hili huanza nyumbani. Tunapotafuta kuwadhuru wenzi wetu, tunajidhuru wenyewe tuwe tunafahamu au la. "*Hao wawili watakuwa mwili moja"* (Waefeso 5:13)

Upendo ni matokeo ya ndoa iliyofanikiwa. (1 Wakorintho 13) upendo sio mwanzo wa msingi wa ndoa kwa sababu njia ya pekee ya mtu kuweza kupenda kama 1 Wakorintho 13 inavyoeleza ni kupitia majaribu na furaha ya maisha ya kila siku pamoja na mwingine na kukubali jinsi tunavyotakiwa na Mungu.
Soma 1 Wakorintho 13:4-8 Tazama sifa za upendo wa Mungu. Zinazalishwa ndani yetu na Mungu tunapokubali kikamilifu mwenzi katika ndoa. Watu waliojenga ndoa yao mwanzoni juu ya upendo, kulingana na jinsi ulimwengu unapouelewa, hawajapitia kinachomfanya Mungu kukuza sifa hizi ndani yao. (Wakati wa kuchumbiana tunadhihirisha sifa zetu nzuri. Hujamjua mwenzako wakati huu.) Ndoa iendeleapo mapenzi yanakuzwa.Watu huanza kuona upendo wa Mungu ukienenda katika nyumba wakikubali kikamilifu.

Wanaume wote huathirika kwa njia inayofanana kwa viwango tofauti. Wanawake nao pia huathirika kwa njia inayofanana kwa viwango vinvyotofautiana. Watu waliojitolea kupenadana kama inavyodhihirika katika ndoa ya kiungu, watatafuta kudhihirisha yaliyo mazuri katika wenzi wao wa ndoa.

*"Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja. Siri hiyo ni kubwa; ila mimi nanena habari ya Kristo na kanisa. Lakini kila mtu ampende mke wake kama nafsi yake mwenyewe, wala mke asikose kumstahi mumewe."*

©1983, Dr. Randy Brodhagen, Glory To God Ministries International™,
all rights reserved